# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 202
# GREDI YA 6 – KISWAHILI INSHA
# Muda: Dakika 40

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Andika insha kama ulivyoelekezwa.

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

**SEHEMU A: UFAHAMU**

**Umepewa dakika 40 kuandika insha yako. (alama 20)**

**<u>MWALIMU MKUU WA SHULE YANGU</u>**

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**HUU NDIO UKURASA WA MSWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

***Mwongozo wa kusahisha***
***INSHA: MWALIMU MKUU WA SHULE YANGU***

Mwalimu mkuu wa shule yangu ni kiongozi muhimu sana ambaye huiongoza shule yetu kwa bidii na hekima. Yeye hufanya kazi yake kwa kujitolea kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata elimu bora na mazingira mazuri ya kujifunzia.

Mwalimu mkuu huhakikisha kuwa walimu wanafundisha ipasavyo na wanafunzi wanafuata sheria za shule. Pia huhakikisha kuwa nidhamu inazingatiwa ili kuwe na amani shuleni. Ameshirikiana na wazazi na walimu wengine ili kuboresha maendeleo ya shule yetu.

Aidha, mwalimu mkuu hututia moyo wanafunzi kufanya bidii katika masomo yetu. Hutuonya kuhusu tabia mbaya kama vile uvivu, utoro na uharibifu wa mali ya shule. Hii imesaidia wanafunzi wengi kuboresha matokeo yao.

Kwa ujumla, mwalimu mkuu wa shule yangu ni mfano bora wa uongozi na nidhamu. Tunampenda na kumheshimu kwa kazi yake nzuri ya kuendeleza shule yetu.

***RUBRIKI***

**Kichwa: “Mwalimu Mkuu wa Shule Yangu”**
**Jumla: Alama 20**

## 1. MAUDHUI (ALAMA 8)

- 7–8: Maudhui kamili, yanahusiana na mada, mawazo yamepangwa vizuri na yanaeleweka.
- 5–6: Maudhui mazuri lakini kuna upungufu mdogo wa mifano au mpangilio.
- 3–4: Maudhui ya wastani, mawazo hayajakamilika au yana kurudia.
- 1–2: Maudhui hafifu sana, hayahusiani sana na mada.
- 0: Hakuna maudhui yanayoeleweka.

## 2. LUGHA (ALAMA 6)

- 5–6: Lugha fasaha, sarufi sahihi, msamiati mzuri.
- 3–4: Makosa machache ya sarufi na tahajia lakini maana inaeleweka.
- 1–2: Makosa mengi ya lugha yanayoathiri uelewa.
- 0: Lugha haieleweki.

## 3. MPANGILIO (ALAMA 4)

- 4: Aya zimepangwa vizuri, mtiririko mzuri wa mawazo.
- 3: Mpangilio mzuri lakini kuna kasoro ndogo.
- 2: Mpangilio dhaifu, aya hazijaandikwa vizuri.
- 1: Hakuna mpangilio mzuri.
- 0: Hakuna muundo wa insha.

## 4. UANDISHI NA USAFI (ALAMA 2)

- 2: Uandishi safi, unaosomeka vizuri.
- 1: Uandishi wa kawaida lakini kuna uchafu mdogo.
- 0: Uandishi mbaya sana au haueleweki.

***JUMLA: ALAMA 20***